# TUME YA RAIS YA PAMOJA YA USIMAMIZI

SMZ
SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

## SEMINA YA VIONGOZI WA VYAMA VYA SIASA

BWAWANI HOTEL, ZANZIBAR
27 – 28 APRILI 2002

# UVUMILIVU WA KISIASA NDANI YA DEMOKRASIA YA VYAMA VINGI

Na: Dk. Salim Ahmed Salim

# UVUMILIVU WA KISIASA KATIKA MFUMO WA VYAMA VINGI

**NA**

**SALIM AHMED SALIM**

Napenda kutanguliza shukrani zangu kwa Tume Ya Rais Ya Pamoja Ya Usimamizi kwa kunikaribisha niweze kushiriki katika Semina hii yenye umuhimu wa pekee, na pia kwa kunipa fursa ya kuchangia mawazo katika suala hili ambalo ni mhimili wa mustakabali wetu kama Watanzania, na kama Waafrika, katika medani ya maendeleo ya ulimwengu wa kisasa.

Ninawapongeza na kuwashukuru kwa dhati wajumbe wa Tume kwa kubuni wazo la kuandaa Semina kama hii. Kwa hakika, ubora wa mkusanyiko huu, hauishii tu katika umuhimu wa suala linalozungumziwa, bali unadumishwa zaidi na kile kitendo cha kutuweka pamoja sisi sote kama Watanzania, pamoja na mitazamo yetu tofauti ya kisiasa, tukatafakari ni nini kiini na msingi wa hatima yetu. Ni dhahiri, mafanikio ya Semina hii ni kielelezo cha mpevuko wa jamii yetu kisiasa na ;pia ni msingi wa kujenga utamadumi unaotujumuisha sisi sote na kuimarisha maslahi yetu na ya vizazi vyetu vijavyo.

Aidha, ninawapongeza washiriki wote wa Semina hii mliofanikiwa kufika hapa Bwawani Zanzibar. Kuitikia kwenu wito wa Tume Ya Rais Ya Pamoja Ya Usimamizi kunadhihirisha jinsi mnavyoliltilia maanani suala hili la kuvumiliana na mnavyolipa kiapumbele katika kujenga mfumo bora wa Siasa na wa maelewano nchin kwetu.

Mada niliyokaribishwa kuizungumzia ni nzito. Uzito wake hauko tu katika kina kinachohitajika kuitafakari, bali pia kwa jinsi suala zima la uvumilivu lilivyokuwa karibu nasi kwa kiasi kikubwa, na jinsi linavyotugusa na kutuathiri katika maisha yetu ya kila siku kama Wanzanzibari, kama Watanzania, na kama Waafrika kwa ujumla.

Mara nyingi, masuala yanayohusu vyama vya siasa huamsha ari na hisia kali, na pia malumbano yenye mvutano katika kuyazungumza. Lakini suala la uvumilivu katika mfumo wa vyama vingi huamsha ari kubwa zaidi, inayozidishwa na kukuzwa na ushabiki wa kisiasa.

Tukiwa tunafahamu hilo, basi ni muhimu sana kuzingatia kwamba kutafakari suala la uvumilivu, katika mkusanyiko wenye mitazamo tofauti ya kisiasa, kwenyewe kunahitaji ustahamilivu. Vinginevyo, azma yote ya kukutana na kutafakari kwa kuchangiana

mawazo kwa dhamiri ya kujenga lengo la pamoja, kutazua ubishi na kushutumiana zaidi kuliko kuelewana. Sidhani kama hilo ndilo lengo la kuwepo kwetu hapa.

Ningependa kukumbusha kuwa nia yetu ya kujumuika hapa Bwawani sio tu kuchambua kisomi suala la uvumilivu, bali ni kujizatiti kwa madhumuni ya kujenga uvumilivu zaidi katika nchi yetu tukiwa katika safari ya kuimarisha demokrasia. Itakuwa kiroja kisiomithilika ikiwa hitimisho la semina ya uvumilivu ni kufumua na kuongeza kutovumiliana !!

Jambo lililo dhahiri ni kwamba kila chama cha siasa kina wajibu wa kujenga utamaduni wa uvumilivu. Utamaduni uwe miongoni mwa viongozi na wanachama kwa jumla wa kuvumiliana wenyewe kwa wenyewe ndani ya Chama husika na baina ya vyama vingine vya siasa.

Ninayasema haya kwa sababu natambua kuwa ingawa Chama cha siasa ni umoja wa watu wenye mawazo na fikra zinazofanana juu ya namna ya kuyatumia madaraka ya kisiasa kuongoza umma, upo uwezekano wa kuwepo tofauti katika mbinu na mikakati ya utekelezaji hata baina ya wanachama wenyewe. Uongozi wa Chama cha siasa ulio makini haustahili kuzifumbia macho wala kuzipuuza tofauti hizi bali

utajitahidi kuandaa mazingira ambamo ingawa kauli ya wengi hatimaye ndiyo hushinda walau wachache nao hupewa haki ya kusikilizwa. Hii ni moja ya kanuni ya msingi kwa wale wanaoamini juu ya umuhimu wa **kujenga demokrasia ndani ya Chama husika.**

Chama ambacho hakikufanikiwa kujenga utamaduni huo wa kuvumiliana na kuheshimiana baina ya wanachama wake hakitoweza kuienzi dhana ya uvumilivu wa kisiasa kinapoingia katika harakati za kisiasa na wapinzani toka vyama vingine. **Badala ya kutegemea nguvu ya hoja kukabili upinzani, nguvu zitaelekezwa zaidi katika kuchochea jazba na hoja ya nguvu.** Ninachotaka kusisitiza hapa ni kuwa uvumilivu wa kisiasa ni muhimu si tu baina ya vyama vinavyohitilifiana kiitikadi bali hata ndani ya kila Chama. Ni utamaduni ambao hauna budi ujengwe ndani ya kila Chama kwa kuzingatia kanuni na misingi ya demokrasia ndani ya kila Chama ambayo imeainishwa katika katiba za vyama.

Ikiwa kila mwanachama muumini wa demokrasia atajenga mazoea ya kuheshimu na kuongozwa katika kauli na matendo yake na katiba ya chama chake, haitokuwa kwake vigumu kuheshimu utaratibu wa aina hiyo uliowekwa kwa mujibu wa sheria kuongoza shughuli za kisiasa katika jamii nzima. **Kwa hiyo**

**kuheshimu katiba iliyowekwa kihalali** ni kanuni nyingine muhimu itakayotuwezesha kujenga utamaduni wa kuvumiliana kisiasa ndani ya mfumo wa siasa ya vyama vingi.

Lakini mambo haya ninayoyasema yanaweza yakaonekana kuwa dhahiri mno kiasi hata cha kutufanya kuamini kuwa hayahitaji jitihada ya kila mmoja wetu kuyafanya yawe ni utamaduni wetu wa kisiasa. Tuisahau wahenga walisema; **"ukiona vinaelea vimeundwa".** Nao uvumilivu wa kisiasa hujengwa kwa jitihada za makusudi na katika kufanya hivyo, yapo matatizo ambayo hayana budi kutanzuliwa. Baadhi yanaweza kutanzuliwa mara moja. Lakini yapo ambayo yatahitaji muda kabla ya kupatiwa ufumbuzi ukitegemea ni kwa kiasi gani yamejizatiti katika mila na desturi au ni urithi wa historia ya jamii. Kikubwa ni kuyatambua kuwa hayo ni matatizo na kikwazo kikubwa katika dhamira yetu ya kujenga mfumo wa kisiasa wenye kutoa fursa sawa kwa wote kushiriki katika uendeshaji wa jamii.

Hadi sasa nimekuwa nikizungumzia chama au vyama kama taasisi. Ni kweli chama ni taasisi, ina muundo, kanuni na taratibu zake. Lakini vilevile chama ni wanachama na katika sura hii ya chama kuwa ni wanachama ndipo kukawa na chimbuko la matatizo.

Wanachama ni binadamu, kila mmoja ana hisia, hulka na matarajio yake. Katika yote haya, upo uwezekano baadhi wakaweka mbele zaidi **ubinafsi** kuliko maslahi ya chama au jamii. Ingawa siyo rahisi kuikana nafsi, lakini ubinafsi ukiwekwa mbele zaidi unaweza ukasababisha upofu wa kutoona mema zaidi ambayo yanaweza kupatikana kwa kutanguliza maslahi ya jamii mbele kuliko hatima ya kila mmoja wetu.

Ni sababu hiyo hiyo ya ubinafsi hata katika maana ya chama hupelekea tushindwe kuona mantiki na ubora uliomo katika hoja inayojengwa na wale tusioafikiana nao kisiasa. Hujiandaa kupinga hoja ilimradi tuipinge tu kwa sababu ni wajibu wetu kuipinga. Mtizamo wa namna hii siyo sahihi kwa chama wala kwa jamii na kwa kweli humfanya hata yule mwenye mtazamo huo aonekane mtu mwenye upeo duni asiyeweza kuona jema ambalo wenzake wanaliona. Si vyema tukajifikisha hapo. Ni kweli kazi ya chama cha upinzani ni kuikosoa serikali kwani bila kuifanya kazi hii watu watapima vipi uwezo wa chama hicho na nini watarajie pindi kikipata ushindi katika uchaguzi? Lakini kazi hiyo ya upinzani ni lazima ifanywe kwa hekima na busara itakayokiwezesha kukijenga chama chenyewe machoni mwa watu. Lakini vivyo ndivyo ilivyo kwa chama kilicho madarakani. Haifai kulikataa kila jambo ilimradi tu limewasilishwa na upinzani. Ni lazima kipambanue upinzani wenye lengo la

kusukuma mbele agenda ya wapinzani wake na kosoa inayotokana na tafsiri sahii ya mstakabali wa taifa.

Katika dunia ya sasa, suala la kuwa na ushindani wa kisiasa limekuwa ni nguzo muhimu na kigezo cha uimara wa demokrasia. Ikiwa hivi ndivyo, haifai kuchukulia tofauti zetu za kisiasa kuwa ni uadui. Wapinzani wa kisiasa si maadui bali wenzetu katika kuimarisha demokrasia na ujenzi wa jamii yetu. Pamoja na tofauti zetu kuna mambo mengi yanayotuunganisha na kubwa zaidi ni kwamba sote ni wazanzibari na sote ni watanzania. Kwa pamoja tunawajibu wa kuijenga Zanzibar kama tulivyo na wajibu wa kuijenga Tanzania. Lengo letu ni kuiona Zanzibar na kwa mantiki hiyo hiyo Tanzania ina amani, utulivu, umoja na mshikamano ambamo kila mtu, bila kubaguliwa ana fursa ya kujiendeleza. Tofauti zetu za kisiasa hazinabudi kuwa chemchemi ya mawazo na mikakati ya kuongeza kasi ya maendeleo ya wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla.

Mwaka 1992 Watanzania tulifanya uamuzi wa kurejea katika mfumo wa siasa wa vyama vingi. Ni uamuzi uliofanyika kuzingatia kupevuka kwetu kisiasa kama jamii na pia kutambua misingi ya mahitaji yetu ya maendeleo kwa kipindi tulichofikia. Wakati huo huo, katika medani za kisiasa ulimwenguni, demokrasia, na

hasa demokrasia ya vyama vyingi, ilichukua kipaumbele. Sisi wenyewe tulikuwa tayari na tuliridhia kwa pamoja kuingia katika mwenendo huo wa kisiasa.

Katika dhamira ya kujenga mfumo wa siasa wa vyama vingi, tulizingatia haja ya kuhakikisha kuwa kila mwananchi anatambulika kuwa ni kiungo muhimu cha jamii, na pia kila mmoja wetu anapata nafasi sawa ya kushiriki katika maendeleo ya nchi yetu.

Aidha uamuzi huo pia ulizingatia umuhimu wa wananchi kuwa na nafasi kamili ya kuchagua na kuhakikisha nani miongoni mwetu anakabidhiwa jukumu la kuongoza serikali na kutuwakilisha katika vyombo mbali mbali vya dola. Na kwa mantiki hiyo, wananchi wanakuwa na uwezo thabiti na uliopangika na kuhalalishwa kikatiba wa kubadilisha uongozi kwa ridhaa ya pamoja.

Kiini cha Mfumo wa vyama vingi ni kuhakikisha kuwa dola inazingatia maslahi ya jamii nzima na sio ya kikundi au sehemu moja ya jamii. Na katika hali hiyo, ndivyo taasisi mbali mbali, zilizomo ndani ya dola au nje, ndani ya serikali au nje yake, zinakuwa na majukumu mbali mbali ya kulinda maslahi ya jamii. Kwa hiyo walio ndani na nje, vyama au vikundi, wote wana dhima kubwa sana kwa jamii.

Vyama vya siasa ni nyenzo ya kuiweka jamii pamoja licha ya tofauti za kimtazamo. Ningependa kusisitiza sana suala hili, kuwa msingi wa mfumo wa vyama vingi vya siasa, ni kutumia vyama kama ni nyenzo za kuwianisha tofauti za kimtazamo ili kudumisha umoja ndani ya jamii. Kwenda kinyume na hivyo, ni kuvuruga maana nzima ya damokrasia ya vyama vingi !

Uvumilivu katika mfumo wa vyama vingi ni kukubali kwa dhati kwamba vyama vya siasa ni vyombo muhimu vya kujenga na kudumisha maendeleo ya nchi – ili mradi vyama hivyo vinaendesha mambo yake katika misingi iliyokubaliwa. Uvumilivu ni kuheshimu jukumu na umuhimu wa vyama vya siasa katika jamii na kutambua kwamba ujumla wake unaainisha nyanja ya mkabala wa tofauti za mitazamo yetu.

Badala ya kuhojiana misikitini, kanisani, sokoni, mitaani, au katika jumuia zetu za kazi au kijamii – tunakusanya mawazo yote hayo na kujumuisha katika uwanja wa vyama vingi ambako ndipo tunapofungamanisha mitazamo yetu. Tukiharibu katika nyanja hizo, basi tutalazimisha tofauti hizo zijitokeze katika maeneo hayo tulizoziondoa, yaani mitaani, kanisani, misikitini, na kadhalika. Vivyo hivyo, tukichanganya masuala yasiohusu siasa – kama dini,

kabila, asili, eneo la mtu atokako na mengineyo kama hayo, basi tutakuwa tunaharibu mfumo mzima wa vyama vingi na msingi wake wa kuleta umoja.

Ningependa kusisitiza kwamba kuheshimu majukumu ya vyama vya siasa katika jamii ni suala linalohusu vyama vyote vya siasa - vilivyoshikilia dola na vilivyo nje ya dola. Hili ni muhimu kuzingatia kwa sababu kazi ya vyama vya siasa na wanachama wake sio tu kutwaa madaraka - bali ni kuchangia katika kufikia mustakabali wa jamii yote kwa taratibu zilizokubalika kwa pamoja. Waliokuwa ndani ya dola wana dhima yao, lakini na waliokuwa nje ya dola nao pia wana majukumu ya lazima katika jamii. Sehemu moja ikiwa dhaifu katika kutekeleza wajibu wake, basi inayoangamia ni jamii yote na sio tu sehemu hiyo.

Ili kufanikisha azma hiyo ya kujenga umoja kwa kuzingatia tofauti za mitazamo yapo mambo muhimu yanayopaswa kuzingatiwa katika mfumo huu. Mwanzo kabisa ni kutambua kuwa msingi wa tofauti za vyama ni sera na hoja. Upinzani wa kisiasa katika mfumo huu haupaswi kujengwa na chuki, visasi, uhasama au mgawanyo tu wa kiasilia. Wakati wote washiriki wa kweli katika mfumo wa vyama vyingi hujenga sera na hoja, na ushindani unakuwa katika nyanja hizo. Yoyote anaekwenda nje ya upeo huo wa sera na hoja, basi

hawaharibii walio katika vyama vingine tu, bali anaivuruga jamii nzima. Kuendesha siasa za chuki au kuongozwa na jazba badala ya hoja ni dalili tosha ya kufilisika kisiasa.

Jambo jingine la kuzingatia ni kwamba uvumilivu katika mfumo wa vyama vingi unaimarishwa na uzalendo – ikimaanisha kudumisha na kuweka mbele maslahi ya jamii wakati wote. Ni kweli, katika muda fulani kutakuwa na chama au vyama tawala, na vyama vya upinzani. Lakini, kama nilivyosema hapo awali, vyama ni nyenzo tu, na haipaswi kuendeleza ushindani ama wa kudhoofisha chama tawala, au kusambaratisha upinzani katika hali ya kuangamiza maslahi ya jamii. Ni ule uchungu wa nchi na watu wake ambao tunasema sote tunao, ndio siku zote unapaswa kututoa munkar na kuendeleza uvumulivu.

Kwani tunapotambua kwamba wote, walio katika utawala na upinzani, ni sehemu muhimu ya demokrasia, na kwamba sehemu moja inapokuwa haipo au dhaifu basi inayoharibikiwa ni demokrasia ya wananchi, utambuzi huo wenyewe unapaswa kutusisitizia umuhimu wa kufanya kazi pamoja, kila mmoja akitekeleza jukumu lake.

Semina hii inafanyika wakati Watanzania kwa jumla na Jumuiya ya kimataifa inafuatilia kwa makini utakelezaji wa muafaka huu. Semina yenyewe ni matokeo ya jitihada za kutekeleza muafaka huu. Ni matarajio yangu kwamba hatutakubali kuyumbishwa katika kuutekeleza. Ni muafaka wetu kwa ajili ya manufaa na ustawi wa Taifa letu. Tuulinde.

Zanzibar hivi sasa kuliko wakati mwingine wowote inayo fursa ya kuonyesha dunia mfano bora wa ukomavu wa kisiasa unaojidhihirisha katika siasa za kuvumiliana na kuheshimiana licha ya matatizo ya hapa na pale. Tuitumie vyema fursa hii.

Napenda kumalizia kwa kukumbusha ule usemi maarufu kwamba 'mstahimilivu hula mbivu'. Usemi huu una mantiki yake katika mazingira ya kawaida na hata yasiyokuwa ya kawaida ya maendeleo ya jamii. Lakini nathubutu kusema kwamba suala zima la ustahamilivu na uvumilivu lina maana ya kipekee na umuhimu wa aina yake katika medani ya siasa yenye lengo la kuimarisha demokrasia ya mfumo wa vyama vingi.

Nchi zetu nyingi katika Afrika zimo katika kipindi cha mpito. Kwa sababu za kihistoria, nyingi miongoni mwa nchi zetu zilikuwa zina mfumo wa utawala wa chama kimoja. Hiyo kwa kiasi fulani inatokana na

vuguvugu la kupambana na ukoloni na kuleta uhuru wa nchi zetu. Bahati mbaya nchi zetu nyingi baada ya kupata uhuru pia zilipata sokomoko ya kutawaliwa na serikali za kijeshi. Kwa hiyo basi kipindi cha mpito cha hivi sasa ambacho kinapamba moto takriban katika nchi zetu zote, ni kipindi ambacho kinazitoa nchi hizi kutoka ama utawala wa chama kimoja au utawala wa kijeshi kwenda katika mfumo wa demokrasia ya vyama vingi. Ili kufanikisha mageuzi haya ni muhimu sana kujenga utamaduni wa uvumilivu na ustahamilivu ambayo ni misingi pekee inayoweza kutuhakikishia kuondokana na malumbano na magomvi ambayo hayamsaidii yeyote.

Naelewa fika kwamba kimsingi ni rahisi kusisitiza mambo haya kimsingi, lakini si jambo jepesi kuyatekeleza kwa vile ni hulka ya binadamu kuendelea na tabia alokwishaizoea kwa muda mrefu. Lakini jambo lililo wazi ni kwamba ni muhimu sana kujenga utamaduni huu na vile vile kuimarisha utamaduni wa amani, utulivu, uelewano na mshikamano, mambo ambayo ni ya msingi kabisa siyo tu katika kuimarisha demokrasia ndani ya nchi zetu za Afrika bali pia katika kusukuma gurudumu la maendeleo la nchi zetu moja moja na Bara letu kwa jumla.